## 14-Nuwn Saakinah Na Tanwiyn

Nuwn saakinah: Ni herufi ya nuwn نْ isiyokuwa na *i'raab* ambayo huthibiti katika kutamkwa, kuandikwa, kusimama na katika kuunganisha.

Tanwiyn: Ni nuwn saakinah iliyozidi inapatikana mwisho wa nomino kwa kutamkwa wakati wa kuunganisha na hutengamana na hiyo nomino wakati wa kuandika na kusimama.

Tofauti baina ya nuwn saakinah na tanwiyn:

| **Nuwn saakinah** نْ | **Tanwiyn** ً ٌ ٍ |
|---|---|
| Inapatikana katikati ya neno na mwisho wa neno.<br>فَسَيُنْغِضُونَ - وَلَئِنْ | Inapatikana mwisho wa neno pekee.<br>وَكِيلًا |
| Inapatikana katika nomino kitenzi au kihusishi.<br>ٱلْمُنْخَنِقَةُ - يُنفِقُونَ - مِنْ | Inapatikana katika nomino pekee.<br>جُنُودٌ |
| Huthibiti katika kutamkwa na kuandikwa katika hali ya kusimama na kuunganisha<br>وَمِمَّنْ حَوْلَكُم | Hutamkwa wakati wa kuungwa na haithibiti katika kuandikwa hali ya kusimama.<br>عَلِيمٌ قَدِيرٌ<br>Mfano unapounga swifah mbili hizo za Allaah (سبحانه وتعالى), utasoma: عَلِيمُنْ قَدِيرٌ. Na ukisimama katika عَلِيمٌ haitakiwi kusomwa عَلِيمُنْ bali iwe عَلِيمْ. |

Hukmu za Nuwn Saakinah na Tanwiyn

| | | | |
|---|---|---|---|
| الإخْفاء | الإقْلاب | الإدْغام | الإظْهار |
| **Al-Ikhfaa** | **Al-Iqlaab** | **Al-Idghaam** | **Al-Idhwhaar** |